

**MTIHANI WA MWIGO**  
**KARATASI YA KWANZA 1 (1013/1)**  
**MUDA: SAA 2**

**JINA LA MTAHINIWA:** .....

**NAMBARI:** .....**DARASA:**.....

**MAAGIZO:**

1. Andika jina lako na nambari katika nafasi ulizoachiwa.
2. Mtihani huu una sehemu NNE muhimu: Insha, Ufahamu, Matumizi ya lugha na Sajili ya lugha.
3. Fuata maagizo uliyopewa mwanzoni mwa kila sehemu
4. Andika majibu yako katika kijitabu hiki.

**KWA MATUMIZI RASMI**

<b>SEHEMU</b>	<b>SWALI</b>	<b>UPEO</b>	<b>ALAMA</b>
1	1	20	
2	2	20	
3	3	30	
4	4	20	
	5	10	
	JUMLA	100	

**SEHEMU YA KWANZA**

1. Andika Insha isiyopungua maneno 350 kuhusu mojawapo ya mada zifuatazo.
  - (a) Ukiwa mkereketwa wa masuala ya siasa na maendeleo, andika hotuba yako juu ya njia bora za kuliendeleza eneo lako la ugatuzi.
  - (b) Ugaidi ni tatizo sugu ulimwenguni kote. Fafanua njia kumi za kukabiliana nao nchini.
  - (c) Maliza kwa: “Iliniwia vigumu mno kuamini jinsi Abdi alivyokuwa amejipunguzia heshima”.
  - (d) Andika insha kuhusu methali ifuatayo, “Kelele za chura hazimzuii ng’ombe kunywa maji”.

## **SEHEMU YA PILI: UFAHAMU ( ALAMA 20)**

2. Soma habari ifuatayo kasha ujibu maswali.

Chumo alikuwa mpenda masomo tangu utotoni. Kila mara alikuwa akiota ndoto za kuwa daktari mashuhuri.. Alijithahidi masomoni hadi akafika chuo kikuu. Hatimaye akafuzu na kuwa daktari.

Baada ya kufuzu, alijikuta akiitwa huku na kule na waajiri wengi. Mwishowe aliangukia kwenye hospitali maarufu nchini. Huko Chumo alilijenga jina lake vilivyo. Utendakazi wake uliwavutia wengi. Wagonjwa wa karibu na wa mbali walimjia kwa utabibu wake mwafaka.

Kadiri miaka ilivyokwenda, ndivyo umaarufu wa Chumo ulivyozidi. Akaona ni afadhali kujianzishia zahanati. Waliokuwa wagonjwa sana wakawa wateja,. Nao wakazidi kumiminika kwake . Chumo aliendelea kuuimarisha ujuzi wake wa matibabu. Akaweza kupambana na maradhi sugu na yale mapya. Sifa zake zikaenea hadi ng'ambo. Jinsi umaarufu wake ulivyozidi ndivyo alivyoingwa na kiu ya mali. Tamaa ikamtambalia. Akaanza kutafuta mbinu za kilaghai za kujilimbikizia mali. Roho yake ya mkonge haikutambulika. Wagonjwa wakaendelea kumwendea. Katika hizo pilkapilka zake za kutafuta matibabu mapya aligundua dawa mujarabu, lakini akaona kama angezitumia wengi wangemwambaa. Akawa na hadhari akawaponya; akawapa dawa kionjesho.

Epuu, kifungua mimba wa Chumo aliamua kufuata nyayo za babayake. Alipofuzu katika fani ya udaktari, aliamua kusaidiana na mvyele wake kazini ili apae kurithi ujuzi. Kweli mwana wa mchunzi asiposana hufukuta.

Wakati Fulani Chumo alipokuwa safarini, Epuu alipata fursa ya kukutana na baadhi ya wagonjwa wa babake. Wengi walionekana kuvunjika moyo waliposikia kuwa daktari kasafiri. Daktari Epuu alizisoma nyuzo zao zilizoonyesha shaka akajisemea, “Vijana tuna taabu. Jamii itathamini ujuzi wetu lini? Bila kufa moyo, aliwahudumia wagonjwa bila kinyongo. Alizisoma faili zao.

Akashangaa ni kwa nini babake alikuwa hajawapa dawa maalum ambazo zingewaponya. Akawapa dawa mwafaka polepole wagonjwa wakaanza kupata nafuu. Baadhi yao wakasikika wakisema, “Kumbe kizaliwacho kinaweza kuwa bora kuliko kilichozaa!”.

Chumo aliporudi kutoka safarini alikuta mambo yamebadilika. Akajiuliza “Mbona chumo limekwenda chini? Kijana amefanya nini? ameshindwa na kazi? mbona wateja hawaji tena? ama wameudhika kwa kukawia kwangu kurudi?” Chumo akaendelea kushangaa wakati alipowapigia simu wagonjwa wake wa hapo awali. Wengi walimwambia walikuwa tayari wamepona. Wakatoa sifa nzuri za kijana.

Chumo alipomhoji Epua aligundua kuwa wagonjea walikuwa wamepewa maibabu kamili. Mzee alimweleza mwanawe kuhusu mbinu ya dawa kionjesho na kuwa tonge limekosa kitoweo. Epua alishika tama akiwaza.

- (a) Taja mafunzo yanayojitokeza katika aya mbili za kwanza. ( alama 3)
- (b) Kwa kurejelea kifungu, eleza jinsi Chumo alivyojiendeleza kikazi. ( alama 4)
- (c) Maana ya methali, “Mgema akisifiwa tembo hulitia maji” Imeadhihirikaje katika kifungu? ( alama 3)
- (d) Taja mambo manne yanayoonyesha kuwa ujuzi wa vijana haukuthaminiwa. ( alama 4)
- (e) ‘Epua alishika atama akiwaza’ inaonyesha kuwa.....(alama 3)
- (f) Eleza vifungu vifuatavyo vya maneno kama vilivyotumiwa katika ufahamu. ( alama 3)
  - (i) Waliokuwa wagonjwa sasa wakawa wateja.
  - (ii) Dawa mujarabu
  - (iii) tonge limekosa kitoweo

**SEHEMU YA TATU: MATUMIZI YA LUGHA ( ALAMA 50)**

- 3. (a) Andika mifano ya sauti zenye sifa zifuatazo: ( alama 2)
  - (i) kipasuo cha kaaka laini
  - (ii) Nazali ya ufizi
- (b) Tumia mzizi “ngali” kutunga sentensi kuonyesha : ( alama 2)
  - (i) Kitenzi

- ii) Kitenzi kishirikishi
- (c) Onyesha maana za “ni” zilizopigiwa ( alama 2)  
Mstari ( alama 2)  
Tokeni darasani
- (d) Tumia neno haraka katika sentensi kama: ( alama 2)
- (i) Nomino \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_
- (ii) Kielezi \_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_
- (e) Tunga sentensi moja yenye kishazi huru na kishazi kitegemezi. (alama 2)
- (f) Andika maana mbili za sentenzi hii: ( alama 2)  
Nenda ukamwone mwenyewe, usiogope
- (g) Tunga sentensi moja iliyo na shamirisho kipozi, kitondo na ala. ( alama 3)
- (h) Maneno haya yako katika ngeli gani? ( alama 2)
- (i) ridhaa \_\_\_\_\_
- (iii) Pacha \_\_\_\_\_
- (i) Akifisha sentenzi hii kwa njia tatu tofauti. ( alama 3)  
Sikujua alikuja jana
- (j) Andika katika usemi wa taarifa (alama 3)  
“Nimemjengea nyumba nzuri akafurahi. Naomi aliwaambia marafiki zake.
- (k) Tunga sentensi katika wakati uliopita hali timilifu. ( alama 2)
- (l) Changanua sentenzi hii kwa njia ya jedwali (alama 5)  
Mwanafunzi atakayeiba mtihani, ataadhibiwa vikali sana.
5. (a) Andika visawe vya maneno yalipogiwa mstari. ( alama 2)  
Mama alivaa mavazi ya rangi ya nili akavutia.
- (b) Methali ifuatayo inatoa ushauri gani?  
Kumcha Mungu si kilemba cheupe. ( alama 2)
- (c) Watu hawa hufanya kazi gani? ( alama 2)
- (i) Mnyapara
- (ii) Sarahangi
- (d) Godoro ni kwa kitanda na zulia ni kwa \_\_\_\_\_( alama 1)

- (e) Toa maana ya: Shika kani ( alama 1)
- (f) Andika maana mbili za neno mlango. ( alama 2)
- (g) Mkono wa saa huitwa \_\_\_\_\_ ilhali mkono wa jembe huitwa \_\_\_\_\_ ( alama 2)
- (h) Haya ni maumbo gani? ( alama 2)
- (i) Mstatili \_\_\_\_\_
- (ii) Pia \_\_\_\_\_
- (i) \_\_\_\_\_ ni ugonjwa wa kuanguka na kuzimia kwa muda. (alama 1)
- (j) \_\_\_\_\_ ni mdudu anayeruka usiku na hufanana na kipepeo. ( alama 1).
- (k) Nambari katika hesabu ambazo zinaweza kugawanyika na mbili bila kubaki kama vile, mbili, nne, sita, nane na kadhalika huitwaje? \_\_\_\_\_ (alama1)
- (l) Andika kwa akisami: Ushuru tatu \_\_\_\_\_ ( alama 1)
- (m) Malipo anayotoa abiria kwa ajili ya kusafiri katika basi huitwa \_\_\_\_\_ (alama 1)
- (n) Kosa la uhalifu huitwa \_\_\_\_\_ (alalama 1).

**SEHEMU YA NNE: SAJILI YA LUGHA (ALAMA 1)**

5. (a) Umepewa jukumu la kuwazungumzia vijana wenzako kuhusu umuhimu wa uwekezaji; Fafanua sifa tano za lugha utakayoitumia. (Alama 5)
- (b) Eleza sifa tano za sajili/lugha katika kituo cha polisi kwenye sehemu ya mapokezi. ( alama 5)